

## Kumbuka

Kupunguza kuhara kwa ndama wa ngamia tumia:

1. Dawa zilizokubalika.
2. Kumwongezea maji mwili kwa kutumia asali, chumvi, na maji.
3. Mayai ya kuku kupitia mdomo kila siku.



**Kuzuia kuhara kunaongeza ndama**



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: [resource.centre@kari.org](mailto:resource.centre@kari.org)

Tovuti: [www.kari.org](http://www.kari.org)

#### Watayarishaji:

Kuria S.G., Tura I. na Walaga H.K.

#### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Marsabit

S.L.P.147, Marsabit

Simu: 069 2040

Nukulishi: 069 2220

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 73 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

## Jinsi ya kupunguza kuhara kwa ndama wa ngamia



## Utangulizi

Kuhara kwa ndama wa ngamia kunasababishwa na virusi pamoja na malisho mabaya na huweza kusababisha kati ya asilimia 12 hadi 60 ya vifo vya ndama walio kati ya mwezi 1 na 3.

Njia nyingi zinazotumiwa ili kutibu kuhara hazitoshelezi lakini njia zifuatazo zinazokubalika na zingine za kiasili zimethibitishwa kuwa za kutosheleza.

### 1. Madawa yaliyokubalika

Tumia dawa yenye madini ya salfa kama vile tembe za *S-dime* kwa mujibu wa maelekezo ya mtengenezaji.



**Mfugaji wa kuhamahama akionyesha tembe ya *S-dime***




**Kutumia *S-dime* kwa ndama anayehara**

### 2. Kutumia mseto wa asali, chumvi ya kawaida na maji

Chukua asali vijiko 3 na chumvi ya mezani kijiko kimoja na nusu kisha uchanganye na lita 3 za maji. Mpe ndama kipimo cha mililita 300 za mseto huu kila baada ya masaa manne hadi kuhara kukome. Njia hii inamponya ndama na pia kumwongezea maji mwilini.



**Kuchanganya viungo**



**Kumpa kupitia mdomo**

### 3. Kutumia mayai

Mayai ya kuku huweza kuponya na kuzuia kuhara kwa ndama. Kwa kupitia mdomo, mpe ndama yai moja kila siku hadi kuhara kukome.



**Kumpa yai kupitia mdomo**